

MAELEKEZO NAMNA YA KUJAZA FOMU YA USAJILI WA KAYA ZENYE WALENGWA

Jina la Fomu	Usajili wa kaya zenye walengwa.
Utambulisho wa Fomu	Fomu Namba 01.
Madhumuni ya Fomu	Kusajili kaya zenye walengwa.
Mahali fomu itakapotumika	Kaya.
Mtekelezaji /Mtumiaji wa fomu hii	Mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji.
Chanzo cha takwimu	Watu wanaoishi kwenye kaya.
Utaratibu wa kukusanya	Mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mradi.
Namna ya usimamizi na uwasilishaji	Baada ya fomu hii kujazwa na kuihakiki, nakala moja ibaki kwa mhudumu wa afya ngazi ya kijiji, na nakala nyingine ipelekwe kwa msimamizi wa wahudumu wa afya ngazi ya kijiji.
Hatua za ujazaji wa fomu hii	Kumbuka: Taarifa zote za kaya katika fomu hii zijazwe kwa herufi kubwa.
	1. Hakikisha unajaza kwa usahihi maelezo yaliyoko juu ya fomu hii ikiwa ni pamoja na tarehe ya usajili, mkoa, wilaya, kata, kijiji/mtaa na kitongoji na utambulisho wa kaya.
	2. Andika jina la mhudumu wa afya ya jamii ngazi ya kijiji na namba ya simu ya kiganjani, kama ikitokea hana simu basi acha wazi.
	3. Andika jina la mkuu wa kaya, pamoja na jina la mke au mume wa mkuu wa kaya.
	4. Andika namba ya simu ya kiganjani ya mkuu wa kaya, pamoja na namba ya simu ya mume/mke wa mkuu wa kaya, lakini ikitokea mkuu wa kaya au mume/mke hana simu, andika mojawapo.
	5. Safu (1): andika majina ya wanaoishi kwenye kaya.
	6. Safu (2): weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku kuonyesha jinsi ya mkuu wa kaya, pamoja na jinsi ya mke/mume wa mkuu wa kaya.
	7. Safu (3, 4, 5, and 6): weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku kuonyesha jinsi yakila mtoto mwenye umri kuanzia miezi 0 hadi 59. kama ikitokea hakuna mtoto mwenye umri katika kundi hili basi usijaze chochote.
	8. Safu (7 and 8): weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku kuonyesha jinsi ya kila mtoto mwenye umri kuanzia miaka 5 hadi 19. kama ikitokea hakuna mtoto mwenye umri huu kwenye kaya acha wazi .
	9. Safu (9): weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku kuonyesha jinsi ya watu wazima wanaoishi kwenye kaya wenye umri kuanzia miaka 20 na zaidi.
	10. Safu (10): safu hii ni kwa ajili ya kina mama wajawazito, weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku kama mama ni mjamzito na anaishi kwenye kaya husika
	11. Safu (11): weka alama ya vema, ✓ kwenye kisanduku ikiwa mlengwa/walengwa katika kaya wana hali ya ulemavu. alama za vema ziwekwe kuonyesha jinsi za walengwa. zingatia: ulemavu uwe ni ule ambao unaweza kuuthibitisha kwa macho, mfano ulemavu wa viungo kama mikono, miguu, ngozi, n.k
	12. Jumla: jumlisha alama zote za vema, ✓ kwenye visanduku kwenye safu zote kisha andika jumla yake kwenye mstari wa chini ulioandikwa jumla.
Uhakiki wa fomu	Hakikisha taarifa zote zimeandikwa kwa usahihi, kabla ya kuondoka kwenye kaya. Hii itarahisisha zoezi wakati wa kufanya majumuisho na kuingiza taarifa katika mfumo wa kompyuta.

